



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**  
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji  
P.O. BOX 01,  
LOLIONDO  
Tarehe 1/04/2022

Nukuu ya bei namba :LGA/005/2021/2022/SHC/W1/ LOT 1 HADI 3  
Ujenzi katika Zahanati ya Sale

**1. TANGAZO LA MWALIKO WA NUKUU YA BEI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea fedha katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ili kugharamia ujenzi wa majengo matatu katika kituo cha Afya Sale. Njia ya ununuzi itakayo tumika wakati wa Ujenzi ni Force Account kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi ya njia kwa mujibu wa kanuni na.167 ya ununuzi wa umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ngorongoro chini ya sheria ya manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia wananchi,makampuni na taasisi mbalimbali kuomba kazi za ufundi katika ujenzi wa majengo matatu kama yalivyo ainishwa hapa chini, kwa ufafanuzi ufuatao.

**LOT 1 UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI 3 IN 1**  
**LOT 2.UJENZI WA JENGO LA MIONZI**  
**LOT 3.UJENZI WA JENGO LA KUFULIA**

**2. MASHARTI MUHIMU YA ZABUNI**

**i) Awe Raia wa Tanzania na pia fundi mzoefu katika kazi za serikali**

**ii)Awe na cheti cha ufundi wa kazi husika kutoka VETA au taasisi nyingine zinazotambuliwa na serikali**

**iii)Muombaji aambatanishe barua ya utambulisho wa ukazi kutoka kwa mtendaji wa Kijiji/mtaa anapoishi**

iv) Muombaji ambaatanishe nyaraka inayo onyesha uzoefu kwa kipindi kisichopungua miaka miwili au zaidi

v) Muombaji awe na uwezo, uzoefu wa kusoma Ramani /Mchoro.

vi) Muombaji aonyeshe bei ya kujenga jengo husika

vii) Waombaje wawe wamesajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA)

### 3. MAELEKEZO MENGINE MUHIMU

i) Fomu za nukuu za bei zinapatikana katika ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni S.L.P 1 Loliondo, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

ii) Ramani/mchoro na nyaraka za zabuni zinapatikana katika ofisi ya manunuzi ya umma Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, muda na Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 7/4/2022 saa 5;00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa tarehe 7/4/2022 saa 5.30 asubuhi kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Waombaji au Wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi

iii) Maombi yanatakiwa kutumwa siku za kazi kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonyesha aina ya zabuni inayo ombwa bila kuwa na viashiria vyovyote vya inakotoka na yatumwe kwa anuani ifutayo;

KATIBU WA BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO  
S.L.P 1  
LOLIONDO



DR. JUMAA MHINA  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
NGORONGORO